# MKATABA WA KUPANGA SEHEMU YA KUEGESHA MAGARI

KATI YA

KALINONE MAULID KALINONE

NA

Chrispell General Supplies & Logistics Limited

2025

**MKATABA WA PANGO WA SEHEMU YA KUTUNZA MIZIGO**

Mkataba huu umeandikwa leo tarehe 17/05/2025 kati ya:

Bw. KALINONE MAULID KALINONE, wa S.L.P 373, Kasulu (hapa atajulikana kama "Mpangishaji"),

NA

CHRISPELL GENERAL SUPPLIERS & LOGISTICS LIMITED, kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania, yenye S.L.P 373, Kasulu (hapa itajulikana kama "Mpangaji").

**1. MAELEZO YA SEHEMU**

Mpangishaji anakubali kumpangisha Mpangaji sehemu yake iliyoko Kasulu kwa ajili ya kuegesha magari na kutunzia mizigo, kwa makubaliano ya mkataba huu.

**2. MUDA WA PANGO**

Muda wa mkataba huu ni miaka mitatu (3) kuanzia tarehe 17/05/2025 hadi 16/05/2028.

**3. KODI YA PANGO**

Mpangaji atalipa kiasi cha Tsh 150,000 (shilingi laki moja na hamsini elfu) kwa mwezi, sawa na Tsh 5,400,000 kwa miaka mitatu ambazo zitalipwa leo muda wa kusaini mkataba huu.

**4. MALIPO**

Mpangaji amekwishalipa kiasi hicho cha Tsh 5,400,000 kwa mpangishaji kwa awamu moja kabla ya kuanza kwa mkataba huu. Mpangishaji anakiri kupokea malipo hayo kikamilifu.

**5.MA TUMIZI YA ENEO**

Mpangaji atatumia sehemu hiyo kwa ajili ya kuegesha magari na kutunzia mizigo tu, na si kwa matumizi matumizi mengine bila idhini ya maandaishi ya Mpangishaji.

**6.MAJUKUMU YA MPANGAJI**

- Kudumisha usafi wa eneo alilopanga.
- Kutolifanya eneo hilo kuwa hatarishi kwa usalama au afya.
- Kutoliharibu au kubadili miundo bila ridhaa ya maandishi ya Mpangishaji.

**7. KUVUNJIKA KWA MKATABA**

Mmoja wa wahusika anaweza kuvunja mkataba huu kabla ya muda kumalizika kwa kutoa taarifa ya maandishi ya miezi mitatu (3) kwa upande mwingine, isipokuwa kwa sababu ya ukiukwaji mkubwa wa masharti.

**8. MIGOGORO**

Pande zote mbili zimekubaliana kuwa iwapo kutatokea mzozo kuhusu mkataba huu, watautafuta suluhisho kwa mazungumzo. Ikiwa haitazaa matunda, shauri hilo litaweza kupelekwa kwa mamlaka husika au mahakama kwa uamuzi.

**9. MKATABA KAMILI**

Mkataba huu unahusisha makubaliano yote kati ya pande hizo mbili na unabatilisha makubaliano yoyote ya awali ya mdomo au maandishi kuhusu jambo hili.

KUTOKA NA KUSAINIWA NA WAHUSIKA HAPO CHINI:

Imetiwa saini mbele yangu na

Innocent Irambona (Director) ........................................

~~Ambaye~~ namfahamu/alietambulishwa

kwangu na BARAKA MAULID KALINOME .........

Ambae ninamfahamu leo tarehe 17/05/

2025

.................... MPANGAJI

Jina: KALIMUNDA VENANCE YUGALUA ..........

Sahihi: ..................

KALIMUNDA VENANCE YUGALUA ADVOCATE, NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P.O. Box 18, KASULU - KIGOMA

Tarehe: 17-05-2025 ..................

Wadhifa: Wakili ..................

Imetiwa saini mbele yangu na

Kalinore Mautid Kalinore.

Ambaye namfahamu/~~alietambulishwa~~

kwangu na ……–……

Ambae ninamfahamu leo tarehe …17…/…05…/

2025

……Kalo……

MPANGISHAJI

Jina: KALIMUNDA VENANCE YUGALLA

Sahihi: ……[signature]……

Tarehe: 17-05-2025

Wadhifa: Wakili.

KALIMUNDA VENANCE YUGALLA
ADVOCATE, NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS
P.O. Box 18, KASULU - KIGOMA